# CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

**DHAHANIA ZA MAKALA ZA KONGAMANO LA MAADHIMISHO YA KUMBUKIZI YA MIAKA19 YA KIFO CHA HAYATI BABA WA TAIFA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE TAREHE 10 NA 11 OKTOBA, 2018**

**MADA KUU: "*FALSAFA YA MWALIMU NYERERE JUU YA TAIFA KUJITEGEMEA NA MAENDELEO YA VIWANDA TANZANIA*''**

**MADA NDOGO*:***

1. **UHURU NA MAENDELEO KATIKA KUELEKEA UCHUMI WA KATI**
2. **MCHANGO WA AZIMIO LA ARUSHA KATIKA MAENDELEO YA VIWANDA**
3. **NAFASI YA ELIMU KATIKA KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA**

**OKTOBA, 2018**

**CHANGING TANZANIA FROM POVERTY TO PROSPERITY**:

*‘‘THE ROLE OF AGRICULTURE IN MAKING INDUSTRIALIZATION A REALITY’’*

Author: Raphael T. Chibunda

Address: P.O.Box 3000 Chuo Kikuu, Morogoro

Email:raphael.chibunda@sua.ac.tz

**Abstract:**

Over the years, history has taught as that the economic difference between developed and underdeveloped countries, is mainly due to the former having higher capabilities in manufacturing, which is synonymous with industrialization. A literature review indicates further that, different countries opt for varying considerations in choosing priority areas on which to centre their industrial policies and strategies. The reasons for making choices range from, market demand, social benefits, security, and many others. In Tanzania after a thorough consideration, the Government decided to choose agro-processing as a cornerstone for Tanzania industrialization strategy.

In this presentation, we are going to discuss the roles of the agriculture sector in fostering industrialization in Tanzania. The presentation will mainly focus on the following critical roles;

- Agriculture will provide the much-needed raw materials for the new industries, as a country we can build a wide range of processing plants for a number of agriculture products like textiles from cotton, leather (hide and skin), beverages, and other agriculture products;
- Produce enough food for workers in the envisaged industries so as to keep under control food-based inflation which tend to hike the cost of living thus increasing the cost of labour and in turn reduces industries’ profitability;
- During the transition period before the new industries start earning enough forex to be used in importation of industrial parts, obviously will depend on forex generated from agriculture produces;
- Improved agriculture sector will increase purchasing power of the local population so that they will be able to purchase the manufactured goods and thus expand the local market;
- Through backward linkages, improved agriculture sector will create more demand for industrial products in form of agriculture inputs such as fertilizers and agriculture machineries, which will result into more industries being established.

Furthermore, the presentation will discuss the current state of agriculture sector in the country and highlights the challenges for modernising agriculture sector and propose the way forward. In conclusion, we are recommending that for agriculture to significantly contribute towards achieving our development goal the country should embark on a major agriculture policy shift, by transforming agriculture from a subsistence activity to commercialized business; increase the application of science and technology in agriculture and formulate a viable and sustainable means of financing the agriculture sector.

# UMUHIMU WA UZALENDO NA UADILIFU KATIKA KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA

Prof. Shadrack Mwakalila.

Mkuu wa Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

***Dhahania***

Rais wa awamu ya kwanza na muasisi wa Taifa la Tanzania Hayati Mwalimu J.K. Nyerere alianzisha viwanda ili kujenga Taifa imara linalojitegemea kiuchumi. Viwanda vilianzishwa vya nguo, kubangua korosho, kuchambua pamba, Zana za Kilimo n.k..Viwanda hivi vilikuwa na manufaa makubwa kwa Watanzania maskini katika sekta ya kilimo.Viwanda hivyo vilijengwa ili viweze kuimarisha uchumi kwa kupata malighafi toka kwa wakulima na kutengeneza bidhaa kabla ya kuuza soko la ndani na la nje ya nchi. Mwalimu aliamini kuwa ili Tanzania iweze kuendelea ni lazima tuwe na viwanda vya kutosha hasa viwanda vya umma kwani uchumi wa viwanda utaliepusha Taifa kuwa tegemezi. Bahati mbaya sana jitihada na mafanikio yaliyofikiwa na Tanzania katika ujenzi wa viwanda hayakudumu kwa muda mrefu. Viwanda vingi vilivyoanzishwa hapa Tanzania vilikufa. Pamoja na mambo mengine sababu kubwa ya kufa kwa viwanda hivyo ni Uongozi na uendeshaji mbaya, hujuma na ukosefu wa uadilifu na Uzalendo. Hivyo, lengo kuu la mada hii ni kuchambua kwa kina falsafa ya Mwalimu J. K. Nyerere juu ya umuhimu wa uzalendo na uadilifu katika kukuza uchumi wa viwanda. Ili kuchambua kwa kina dhamira ya Mwalimu Nyerere katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, mada hii imetumia machapisho mbalimbali ya Mwalimu Nyerere pamoja na machapisho ya watafiti na waandishi mbalimbali. Aidha, kwa kutambua dhamira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya awamu ya tano (5) katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, mada hii imetumia pia machapisho mbalimbali ya Serikali kuonyesha dhamira yake katika kukuza UZALENDO NA UTAIFA na UADILIFU KWA WATUMISHI WA UMMA na UADILIFU KWA SEKTA BINAFSI. Uchambuzi katika mada hii unathibitisha kuwa, ili Serikali iweze kukuza uchumi wa viwanda inahitaji watu ambao ni Wazalendo, Waadilifu, waaminifu, Wenye nidhamu, Wenye kujiheshimu, Wenye mshikamano na wenye kutanguliza mbele maslahi mapana ya Taifa.

# UMUHIMU WA MISINGI YA AZIMIO LA ARUSHA KATIKA KUSTAWISHA VIWANDA VYA NDANI

Dkt. Ayub Rioba.
Mkurugenzi Mkuu
Tanzania Broadcasting Corporation (TBC)
Broadcasting House,
Nyerere Road,
www.tbc.go.tz
ayub.rioba@tbc.go.tz

***Dhahania***

*"Kabla sijaketi, lipo jambo ningelipenda kusema... Pamoja na kutumia kila aina ya silaha dhidi ya umaskini wetu, ni lazima pia tulinde uhuru na heshima ya Jamhuri ya Muungano dhidi ya yeyote anayepanga kutumia mwanya wa shida zetu kutusaidia ili hatimaye awe na nguvu za kututawala"Katu, si misingi yetu, Nchi yetu wala uhuru wetu wa kuamua hatma yetu, viko sokoni kwa ajili ya kuuzwa! (Nyerere, J.K 1968)*

Baba wa Taifa aliyasema maneno hayo (hapo juu) katika Dhifa aliyokuwa amemuandalia mmoja wa viongozi wa nchi marafiki tarehe 4, mwezi Juni, mwaka 1965.

Misingi ya azimio la Arusha imeelezwa katika sehemu mbalimbali ambayo ni pamoja na utu usawa, heshma, haki na ustawi wa wanachi. Kwamba ni wajibu wa Serikali, ambayo ni watu wenyewe, kuingilia kati kwa vitendo maisha ya uchumi ya Taifa ili kuhakikisha ustawi wa raia wote na kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine au kikundi kimoja kunyonya kikundi kingine na kuzuia limbikizo la utajiri kufikia kiasi ambacho hakipatani na siasa ya watu wote kuwa sawa (Azimio la Arusha, uk 2).
Katika kusimamia misingi ya Azimio la Arusha, Serikali kupitia kwa watendaji wake ina wajibu wa kuhakikisha viwanda vinasaidia kuongeza uwezo wa Taifa na watu wake kuwa huru na si vinginevyo.

Vilevile Serikali kupitia kwa watendaji wake ina wajibu wa kuhakikisha viwanda vinajengwa maeneo yote nchini ili kusaidia kupunguza tatizo la ajira;

Pia, kuhakikisha taasisi za utafiti wa masuala mbalimbali ya viwanda zinaimarishwa ili kusaidia uendelevu wa viwanda na teknolojia nchini. Aidha, Lengo kuu la Mada hii ni kuchambua kwa kina falsafa ya Mwalimu J. K. Nyerere juu ya umuhimu wa misingi ya Azimio la Arusha katika kukuza uchumi wa viwanda vya ndani . Katika kuchambua kwa kina dhamira ya Mwalimu Nyerere katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, Mada hii imetumia machapisho mbalimbali ya Mwalimu Nyerere pamoja na machapisho ya watafiti na waandishi mbalimbali.

# UMUHIMU WA TAIFA HURU KUJITEGEMEA KIUCHUMI KATIKA KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA

*Prof.Faustin Kamuzora, Ofisi ya Waziri Mkuu, Dodoma*[1]

## *Dhahania*

Dhana ya kujitegemea kiuchumi, toka ngazi ya mtu binafsi, familia hadi taifa, ni kongwe kama ilivyo historia ya mwana damu. Wanazuoni wa enzi mbalimbali wamefafanua umuhimu wa kujitegemea kiuchumi. Baadhi yao ni pamoja na Lao Tzu, Ralph Waldo Emerson, Johann Wolfgang von Goethe, na Meyerns Keynes. Kwa kutambua kuwa unyonge ndio chanzo cha kushindwa kujitegemea kiuchumi, Mwalimu Nyerere tangu mwanzo wa harakati zake za siasa ya ukombozi hadi mwisho wa maisha yake alipambana kuhakikisha Watanzania na wanyonge wengine wote wanajitegemea kiuchumi. Mathalani, mwaka 1962 aliwaasa Watanganyika kama ifuatavyo: "Hatuwezi kuwa na Uhuru wa kweli ikiwa taifa linajiendesha kwa kutegemea zawadi'.

Katika wasilisho hili mchango wa Mwalimu Nyerere katika kulijenga taifa lenye dhamira ya kujitegemea utachambuliwa ikiwa ni pamoja na sehemu ya tatu ya Azimio la Arusha iliyofafanua siasa ya kujitegema, sera ya elimu ya kujitegemea na uwekezaji katika elimu – tangu kisomo cha watuwazima, elimu ya ufundi hadi elimu ya juu. Mwalimu Nyerere alitambua kuwa rasilimali kuu ya nchi yeyote ni ubora wa maarifa na stadi za watu wake. Yeye binafsi alikuwa mtu wa kutafuta maarifa kwa kujisomea sana na kuandika. Juhudi zake za kuandika zinamfanya kuwa katika Watanzania wachache sana wenye kutunga na kuandika vitabu vingi vinavyosomwa ndani na nje ya nchi.

Wasilisho litakamilishwa na mapendekezo ya aina ya maarifa na stadi zinazohitajika kwa sasa kuweza kujenga Tanzania ya viwanda. Baadhi ya maarifa haya ni pamoja na kujikomboa kifikra, kujiamini, kutambua na kutumia kikamilifu fursa za kuzalisha bidhaa, huduma, ubunifu / ugunduzi ili kujiongezea kipato halali, na elimu ya fedha (financial literacy). Baadhi ya stadi ni pamoja na kuandaa program za komputa na stadi nyingine za kutumia fursa zitokanazo na maendeleo ya TEHAMA, sayansi na utandawazi. Baadhi ya mikikakati ya kufikia azma hii itajadiliwa kwa ufupi ikiwa ni pamoja na kuboresha mitaala ya ngazi mbalimbali za elimu, kujenga utamaduni wa taifa zima wa kupenda kujifunza wakati wote kama alivyofanya Mwalimu Nyerere na kutoa motisha zaidi kwa watunzi / waandishi wa vitabu na wabunifu / wagunduzi nchini.

[1] Maoni yaliyo kwenye andiko hi lini ya mwandishi mwenyewe,hayawakilishi Ofisi ya Waziri Mkuu.

**MTAZAMO WA MWALIMU NYERERE JUU YA AZIMIO LA ARUSHA NA TAIFA LA KUJITEGEMEA**

Montanus C.Milanzi

(PhD Sayansi ya Menejimenti)

Mhadhiri Mwandamizi

Skuli ya Utawala wa Umma na Menejimenti

Chuo Kikuu Mzumbe, Kampasi Kuu

Barua pepe: mcmilanzi@mzumbe.ac.tz

***Dhahania***

Lengo kuu la makala hii ni kutaka kuhudhurisha ujumbe ambao unaangalia mtazamo ama mitazamo ya muasisi wa tamko la Azimio la Arusha na Taifa la Kujitegemea, yaani Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kujenga taifa lenye sifa mbili yaani taifa lenye kufuata siasa ya ujamaa na siasa ya kujitegemea. Mitazamo hii ni muhimu sana kwetu kujifunza hasa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aghalabu Tanzania inaonekana bado kuwa tuko kwenye hatua ya mwanzo ya maendeleo ya kupanda mbegu kwani wakati halisi wa mavuno bado hatujaufikia.

**Mbinu za kiuandishi:** Mwandishi wa makala hii amesoma na kupitia makala mbalimbali yaliyoandikwa na Hayati Baba wa Taifa pamoja na makala za waandishi wengineo juu ya Tamko la Azimio la Arusha pamoja na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea zilizoandikwa kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 60 hadi sasa. Makala hizo ndizo zimekuwa vyanzo maalum vya kuweza kujua mitazamo ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere juu ya Azimio la Arusha na Taifa la Kujitegemea. Vilevile mwandishi ametumia Muundo wa ***Dirisha la Johari*** pamoja na ***mtindo wa Osgood*** ili kuangalia na kubainisha mitazamo aliyokuwa nayo Hayati Baba wa Taifa juu ya tamko la Azimio la Arusha na Taifa la Kujitegemea.

**Utangulizi**

Makala hii inachimbua na kutasua mitazamo aliyokuwa nayo Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuhusu Tamko/Mwongozo/Tangazona Programu ya Azimio la Arusha lililoafikiwa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha siasa cha ukombozi kiitwacho TANU (Chama Tawala) kwenye Mkutano wake uliofanyika mjini Arusha kuanzia tarehe 26 hadi tarehe 29 mwezi wa Januari mwaka 1967. Siku sita baadaye, yaani tarehe 5 Februari, Serikali ilipitisha na kutamka kuwa Azimio la Arusha ni Tamko rasmi la Serikali.

Azimio la Arusha katika makala hii lilihusishwa na Sera ya chama tawala cha TANU (1954 – 1977) inayoitwa Ujamaa na Kujitegemea. Hayati Baba wa Taifa yeye ndiye mhusika mkuu, mtunzi, muumini na muasisi nambari moja wa tamko lote lililozaa makusudi na maazimio

yaliyoko kwenye Azimio/Mwongozo na Programu inayoitwa Azimio la Arusha. Aidha, makala hii inaonesha kuwa Azimio la Arusha haliwezi kamwe kutenganishwa na siasa inayoitwa Siasa ya Ujamaa fauka siasa ya Kujitegemea. Hivyo basi mitazamo ya Mwalimu Nyerere imetunduiwa na imeangaliwa katika mambo makubwa mawili. Kwanza kwa kufuata muundo wa Osgood mitazamo ya Hayati Baba wa Taifa imeangaliwa kwa kupambanua nguzo kubwa tatu yaani Mtazamo wa Kifikra, Mtazamo wa Kitabia na mwisho Mtazamo wa Kimahusiano. Pili, kwa kutumia mtindo wa Dirisha la Johari tumeweza kupambanua mitazamo ya Hayati Baba wa Taifa kuhusiana na Azimio la Arusha katika nguzo za Kazi-ridhisha, Kazi-husishwa na Taasisi-Husika.

Makala hii imeandikwa na kupangwa katika sehemu kuu tano. Sehemu hizo ni hizi zifuatazo: Baada ya dhahania kilichofuata ni utangulizi ambao umeainisha mambo muhimu ambayo makala hii imetaka kuonesha kwa hadhira yake. Mara baada ya utangulizi sehemu inayofuata ni taarafu ama mada yenyewe inayojuvya mitazamo ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere juu ya sera na siasa ya Chama tawala wakati huo chama cha TANU na juu ya ujenzi wa taifa la kujitegemea. Imeeleza pia jinsi ilivyoweza kupata taarifa juu ya mitazamo hiyo: yaani kwa kutumia muundo wa Osgood pamoja na mtindo wa Dirisha la Johari. Hali kadhalika sehemu hii inaeleza wazi wazi misingi mikubwa ya Azimio la Arusha iliyopandikizwa na Hayati Baba wa Taifa pamoja na usimamizi na uongozi thabiti wa kilichokuwa chama cha ukombozi cha TANU kushika hatamu ya uongozi katika upande wa Tanzania unaoitwa siku hizi Tanzania Bara.

Sehemu ya tatu ya makala hii inadadavua na kuangalia kwa kina maandishi juu ya Azimio la Arusha na mahusiano yake mapana juu ya uundaji wa Taifa la Kujitegemea yaani ujenzi wa siasa ya ujamaa na kujitegemea nchini Tanzania. Vile vile inachambua japo kwa kiasi fulani mitazamo aliyonayo Hayati Baba wa Taifa kuhusu Azimio la Arusha na umuhimu wake katika maendeleo ya nchi na wananchi wake pamoja na uongozi katika Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli. Pia sehemu hii inaangalia juu ya dhana ya Taifa la Kujitegemea kutokana na mitazamo ya Hayati Baba wa Taifa katika wakati huu tulionao kwa vyama vya siasa, serikali na wananchi kwa ujumla.

Sehemu ya nne ni hitimisho ama tamati ya makala hii. Yaani imeweka muhtasari wa kina juu ya mambo yaliyoelezewa katika makala hii na kuweka wazi juu ya ushauri wa kiutendaji ambao vyama mbalimbali vya siasa, wananchi pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waweza kujifunza kutokana na fikra, tabia na mahusiano mazuri aliyokuwa nayo Hayati Baba wa Taifa juu ya Azimio la Arusha na dhana ya Taifa la Kujitegemea. Hakika mitazamo ya Baba wa taifa ni tunu na amali ya kujivunia ambayo kila kiongozi na mwananchi wa nchi hii hana budi kuienzi na kuitumia katika kuleta maendeleo kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Sehemu ya mwisho ina orodha fupi ya vitabu/maandiko rejea ambayo mwandishi wa makala hii ameyasoma kwa kinagaubaga na kuyaangalia wakati wa kuandaa na hatimaye kuandika makala hii.

## ELIMU YA KUJITEGEMEA NI MSINGI WA UJASIRIAMALI KATIKA KUWEZESHA MAENDELEO YA VIWANDA TANZANIA

Binto Mawazo Binto
Mhadhiri na Mkuu wa Idara ya Stadi za Uchumi

Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kampasi ya Kivukoni

**Dhahania**

Duniani mataifa mengi yamejikita katika juhudi za kukuza uchumi katika mukutadha wa maendeleo ya viwanda kwa muda mrefu. Wakati wadau wa maendeleo ya uchumi wakipambana kutafuta njia za kuukuza uchumi kwa ufanisi zaidi, njia ya elimu ya kujitegemea ilionekana kuwa na mchango wa kuridhisha kwa wadau walio wengi ikiwa ni pamoja na mataifa yaliyoendelea. Pia Tanzania ilijikita katika matumizi ya nadharia hii pale Mwalimu alipotangaza rasmi Azimio la Arusha tarehe 5 Februari, 1967; ambapo Mwalimu J. K. Nyerere alitangaza misingi ya siasa ya ujamaa, ambayo chimbuko lake lilikuwa ni elimu ya kujitegemea.

Hata hivyo, wakati nchi nyingi duniani zilifanikiwa katika matumizi ya nadharia hiyo, Tanzania haikufanya vizuri kabisa, kwani pamoja na mambo mengine yaliyojitokeza viwanda vilivyo anzishwa baada ya uhuru hadi kufikia mwishoni mwa 1970s , havikufanikiwa kufanya kazi kwa tija endelevu. Kwa kuwa matokeo haya hayakutegemewa, wadau wameendelea kujikita katika kutafuta suluhisho la changamoto zilizopelekea kushindwa kuendeleza viwanda vilivyoanzishwa kwa gharama kubwa. Ndipo katika miaka ya 1980 mpaka 1990, nchi nyingi katika bara la Afrika na Asia zilijikita katika matumizi ya nadharia ya ujasiriamali kama chachu ya kukuza uchumi hasa kwa kuzingatia maendeleo ya viwanda. Wakati nadharia hii ikisaidia kukuza ufanisi wa maendeleo ya uchumi kupitia nadharia ya maendeleo ya viwanda katika nchi nyingi hasa katika bara la Asia na baadhi ya nchi chache za Afrika. Tanzania imekuwa nyuma kwa kiasi kikubwa katika kuielimisha jamii na kuifanya iweze kuitumia nadharia ya ujasiriamali kama msingi wa maendeleo ya uchumi kupitia maendeleo ya viwanda.

Hali hii inasababisha wataalamu kushindwa kujikita kwa ufasaha katika maeneo yao ya ubobezi ili waweze kutoa mchango ulio na tija. Hivyo hujikuta hawana ufanisi katika maeneo yote wanayoshiriki, na hatimaye kukosa kuridhika na ushiriki wao katika maeneo yote ya ushiriki wao katika kukuza uchumi. Hivyo basi, ni dhahiri kabisa kwamba kuna udhaifu mkubwa katika juhudi zinazofanyika katika kuishi "***Falsafa ya Mwalimu Nyerere Juu ya Taifa Kujitegemea na Maendeleo ya Viwanda Tanzania*.**" Mwenendo huu unaashiria kwa uwazi kabisa uwezekano mkubwa wa kushindwa kufikia uchumi wa kati kwa misingi ya kuchochea maendeleo kwa kutumia nadharia ya maendeleo ya viwanda mpaka ifikapo 2025. Hivyo basi, wasilisho la mada hii linalenga kuchochea jamii iweze kujikita katika ushiriki katika shughuli za kimaendeleo katika misingi inayoakisi "**Elimu ya Kujitegemea kama Msingi wa Ujasiriamali Katika Kuwezesha Maendeleo ya Viwanda Tanzania.**

# NAFASI YA UTAMADUNI WA TAIFA KUJITEGEMEA NA DHANA YA MISAADA TOKA NCHI ZA NJE

Dkt. Jason Nkyabonaki: jason.mnma@yahoo.com : +255784 632888

Chuo Cha Kumbukumbu ya MwalimuNyerere-Zanzibar, Tanzania

**Dhahania**

Mwalimu Julius K. Nyerere mara baada ya Uhuru alifanya jitihada za kujenga nchi ya Tanzania kujitegemea kama taifa huru. Dira na mwelekeo ilikuwa ni kujenga taifa la watu ambao wanafanya kazi na kuzalisha mali kwa lengo la kujitegemea na si kutegemea misaada kama vyandarua vya kuzuia mbu. Azimio la Arusha pamoja na mkakati wa serikali kuanzisha vijiji vya Ujamaa vililenga watu kufanya kazi na kujitegemea. Maendeleo kama tunda la kufanya kazi yalilenga kuwafuata watu mahali walipo na kupitia mifumo hiyo ya uzalishaji mali; basi mtu binafsi na jamii wangejikomboa dhidi ya maradhi, ujinga na umasikini. Utafiti huu ulilenga kupata mawazo ya wananchi juu ya dhana ya kujitegemea na kama bado ina nafasi miongoni mwa jamii. Sampuli ilikuwa ya bahati nasibu na ililenga watu wote kuanzia vijana mpaka wazee. Matokeo ya jumla yameonesha, jamii kwa asilimia kubwa wana dhana chanya juu ya misaada hususani ya vyandarua vyakuzuia mbu. Wanajamii wanadai umasikini umewakumba na hivyo msaada kwao ni mkombozi. Pia, kiwango cha watu kufanya kazi kwa nguvu kama ilivyokuwa wakati wa miaka hiyo ya ujamaa na kujitegemea kimeshuka. Watu wenye umri wa kuanzia miaka 45 walisema vijana walio wengi chini ya miaka 30 hawapendi kufanya kazi za uzalishaji mali bali hupenda kupata pesa kwa ujanja ujanja. Hivyo, utafiti huu unahitimisha kwa kuonesha kuwa jamii ya watanzania walio wengi kwa sasa wangependelea kupata msaada kutoka ughaibuni mfano msaada wa vyandarua vya kuzuia mbu. Hivyo, fikra na falsafa ya mwalimu Nyerere juu ya taifa kujitegemea inazidi kufifishwa na mawimbi mazito katika jamii. Serikali ya awamu ya tano imejijenga katika kauli mbiu ya Hapa Kazi tu, hivyo mtafiti anapendekeza kauli mbiu hii ienezwe kwa nguvu zote kufuta mawazo ya wanajamii kufikiria kupata msaada badala ya kufanya kazi kwa nguvu na kujijengea ustawi katka kipindi hiki nchi inapopaa kuelekea uchumi wa kati.

**UMUHIMU WA ELIMU KWA JAMII KATIKA KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA**

EKWABI W.T MUJUNGU

Mkurugenzi wa Idara ya Elimu kwa Umma,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Dodoma

Baruapepe: dgeneral@pccb.go.tz

Simu: Na. 0262323315 Simu ya bure: 113 Wavuti: www.pccb.go.tz

**Dhahania**

Makala hii inaanza kwa kunukuu maneno ya Baba wa Taifa juu ya elimu ya kujitegemea "*Hata hivyo ni rahisi kutamka kwamba masomo katika shule za msingi na sekondari hayana budi yawaandae vijana kwa maisha na mahitaji ya Tanzania. Lakini kutimiza haya kunataka si mapinduzi ya mipango ya Elimu peke yake, bali hata ya fikra za sasa za wananchi. Na hasa mitihani inapaswa ibadilishwe ifanane na mawazo ya serikali na ya wananchi. Sharti tufahamu kwamba mitihani ina faida zake, kama vile kupunguza hatari za upendeleo na ukabila katika kuchagua watakaoendelea.*" J.K. Nyerere, Elimu ya Kujitegemea 1967

Hakuna nchi duniani inayoweza kuwa na maendeleo ya uchumi bila kuwekeza kwenye rasilimali watu. Elimu inasaidia mtu/watu kujielewa wenyewe na kuielewa dunia au mazingira yanayomzunguka, mfano masoko. Elimu inaimairisha ubora wa maisha ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. "*Give a man a fish and he will eat a day, teach a man to fish and he will eat for a life time*". Laozi-Chinese Philosopher

Elimu ina umuhimu mkubwa sana katika jamii. Kwa mfano, wapo wanaosema elimu ni mtaji. Watu hawa wanakwenda mbali kiasi cha kusema kwamba ukidharau elimu ujue unakaribisha umaskini katika maisha yako. Aidha, Uwekezaji katika elimu maana yake unaandaa ukuaji katika nyanja mbalimbali za kiuchumi**.** Uzoefu unatuonyesha kwamba, nchi zilizowekeza vizuri katika elimu, zimekuwa na maendeleo makubwa ya kiuchumi na pia mwenye taaluma nzuri hulipwa vizuri. Mabadiliko ya nguvu ya soko na ujuzi unaohitajika: Ushindani kati ya mabadiliko ya teknolojia na elimu.

Kutokana na umuhimu wa elimu tunakubaliana kwamba, ushindani wa kidunia katika teknolojia unahitaji watu wenye ujuzi wanaoweza kufikiri kwa haraka na kuwa wabunifu. Nchi inaweza kushindana na kufanikiwa: wekeza mapema katika elimu, mfano Mitaala wekeza kwa umakini ( SMART) wekeza katika ujuzi wenye manufaa (relevant skills) mfano Problem solving skills, communication skills, social skills, personal skills for personal management. Ni muhimu kuangazia matokeo makubwa mfumo wa elimu ulenge katika matokeo unayoyataka/tarajia.mfumo wa elimu upitiwe kila baada ya muda kuona kama bado unafaa. Hivyo, Lengo kuu la Mada hii ni kuchambua kwa kina juu ya umuhimu wa elimu kwa jamii katika kukuza uchumi wa viwanda. Ili kuchambua kwa kina dhamira ya Mwalimu Nyerere katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, Mada hii imetumia machapisho mbalimbali ya Mwalimu Nyerere pamoja na machapisho ya watafiti na waandishi mbalimbali.

# NAFASI YA ELIMU KATIKA KUKUZA VIWANDA VYA NDANI

**Rev. Dkt. Charles Kitima.**

## Dhahania

Maendeleo ya viwanda ni ya lazima katika Taifa lolote lile kwani huwezesha raia kujipatia mahitaji ya muhimu kwa maisha yao. Bidhaa za viwanda huunganisha raia na nchi zingine kibiashara. Muunganiko na ubadilishanaji wa bidhaa hutegemea ujuzi na teknolojia ya nchi inayozalisha bidhaa tafutwa. Kwa hivi msingi wa uanzishaji na ukuzaji wa viwanda ni Rasilimali watu. Hivi uwekezaji wa viwanda huanza na uwekezaji kwenye rasilimali watu ambao ndio mtaji mkuu na usiohamishika (Robert Reich, 264).

Elimu ni chombo cha lazima katika kuleta mapinduzi na mabadiliko endelevu katika mfumo wa uchumi. Uchumi wa viwanda unahitaji kujenga namna mpya ya watu kufikiri na kuishi haya ni mapinduzi ya kiutamaduni yanoyomhusu kila raia. Kuwaingiza watanzania katika uchumi wa viwanda lazima kutumia mfumo wa elimu rasmi na elimu endelevu kwa wale walio watu wazima.

Tutahitaji utashi wa kisiasa na kufanya maamuzi kuwa Tanzania ianze na viwanda vipi na kwa teknolojia ipi na kwa wawekezaji gani na kwa ajili ya masoko yapi tunayotaka tuyashikilie. Maswali haya yataweza kujibiwa kwa njia ya elimu na mijadala ya kitaalamu ili kupelekea kuunda sera na mipango madhubuti ya Tanzania pekee ya viwanda yenye mvuto wa kimataifa. Kwa mantiki hii mfumo wa elimu ya Tanzania ndio utakao jibu uwezekano wa viwanda vya kukuza uchumi na kuifanya Tanzania kuwa moja ya nchi za viwanda kwa dhana ya kisayansi.

Taifa letu lazima LIJENGE MIFUMO imara ya uchumi, fedha, ELIMU, afya, Nishati, Miundo mbinu ya usafirishaji, Mazingira na kujenga mifumo bora ya huduma za kiserikali. Mifumo hii ya umma na miingineyo kama hii huwa nufaisha raia wote kwa kujenga maendeleo yanayo tabirika kwa wananchi walio makini na wachapakazi. Maendeleo haya humvuta kila raia na kuhamasika kujiingiza katika sehemu stahiki ili awe mshiriki na mnufaika.

Nchi zinazo thubutu kusukuma watu wake kukumbatia mifumo tajwa hapo juu kwa sasa zimeanza kuagana na umaskini wa mtu mmoja mmoja na umaskini wa kitaifa. Pato binafsi na pato la Taifa hukua na kuwezesha kujenga kundi kubwa la raia wenye uwezo wa kugharimia (purchasing capacity) mahitaji ya mhimu mf. Kugharamia elimu, teknolojia na afya.

Maamuzi ya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025 ni maamuzi mazuri ila yatakuwa ndoto kama elimu haitamjengea raia uwezo wa kumiliki teknolojia na mtaji. Sekta binafsi inayomiliki viwanda lakini haijaunganishwa na mfumo wa elimu haiwezi kujenga pato endelevu wala utamaduni mpya wa viwanda. Wakati wa Ujamaa tulifanikiwa kujenga sekta ya viwanda ya umma chini ya elimu ya kujitegemea na mfumo wetu wa elimu ukiungana na kila kiwanda na wizara mama. Mafanikio tuliyaona ila tulipoachana na ujamaa tumekosa dira kwa sababu hatuna falsafa ama mfumo wa kufikiri kiuchumi na kiteknolojia. Tuliingia mfumo mpya wa uchumi bila kuandaa jamii na mfumo wa elimu hauoani na mfumo wa uchumi tunaopaswa kuwa nao, mf. Wakulima wa mbaazi wanasubiri serikali iwatafutie masoko japo walilima kwa hiari yao.

Mifumo ya elimu, kijamii na kiuchumi ikiwa shirikishi (inclusive models) hujenga fursa kwa kila raia na kujenga ushindani wa kitaifa katika uchumi wa viwanda duniani. Raia huwa na sauti katika kubaini vitu vya muhimu vya kuweka kwenye mitaala ya elimu msingi na elimu ufundi na ujuzi ambayo ni ya lazima kwa nguvu kazi ya Taifa. Tanzania itakapoamua aina ya viwanda itaamua pia aina ya teknolojia na ujuzi hitajiki.

Jitihada zilizo fanywa kupanua elimu Msingi (Basic education) ni mwanzo mzuri sana kwa Tanzania ya viwanda endapo tutaamua aina ya viwanda na teknolojia tunazotaka kwa bidhaa za masoko lengwa. Kwa sasa watoto wanasoma bila kuunganishwa na mkakati wa viwanda wala soko la ajira duniani. Viwanda vina sura ya kidunia sio ya ki-nchi tu ndio maana nchi kama China, Vietnam na India wameweza kujichotea fursa kemkem kwa nchi za Afrika, wakati Tanzania iliyoshiriki kukomboa nchi hizo haina hata ushirikiano wa kibiashara unaofahamika kitaifa.

Ili Tanzania iweze kuwa na elimu yenye kukuza uchumi wa viwanda vya ndani yafuatayo yangeweza kuwa mwanzo mzuri

1. Kuja na aina ya mahitaji ya masoko ya ndani na nje, mfano. Kuimarisha viwanda vya ndani vilivyo fungamana na VETA.
2. Kuunganisha sekta ya binafsi ya kitanzania na teknolojia kwa ajili ya ushindani wa kimkakati.
3. Mitaala ya Elimu ya awali na Elimu ya Shule ya Msingi ijenge utayari wa kisayasi na ufundi pamoja na uadilifu wa mtoto.
4. Elimu ya sekondari mitaala yake iweke mkazo kwa masomo ya sayansi huku watoto wakizoeshwa kutumia maabara kwa muda mwingi.
5. Elimu ya Msingi iwajengee hamasa vijana kupenda ufundi na ujuzi kwani nusu ya watoto hubaki na elimu ya msingi bila kuendelea na elimu ya utatu (tertiary level). Kabla ya kufikia miaka 18 kwa wale ambao hawakuendelea na elimu ya sekondari iwe LAZIMA kusomea ujuzi maalum (vocational/occupational skills). Hivi tutakuwa na raia wenye ujuzi zalishi (Skilled national workforce). Mafunzo kwa vitendo vichukue nusu ya muda wa elimu ya ufundi kwa wale wanaosomea ufundi.
6. Utafiti: Taifa likae na kuwaza namna maalum juu ya kufikia ukombozi wa kiteknolojia na kiuchumi (Technological and Economic Sovreignity).
7. Elimu ya Uchumi na viwanda kwa watengeneza sera na wafanya maamuzi ikiwahusisha raia wote ni muhimu sana. Kuna ombwe na tatizo kubwa kati ya watanzania wanakotaka kwenda na mwelekeo wa wizara. Nchi makini kwa mfano haingezibia watoto wa maskini fursa za elimu ndani ya nchi na kuwasababisha waitafute elimu ya juu ya awali wakasomee nje.
8. Elimu ya Juu katika nyaja zote ilenge mfumo wa uchumi wa kiushindani kimataifa.
9. Elimu yetu iandae vijana wetu kuongoza Afrika kiuchumi kama tulivyoandaliwa kukomboa Afrika dhidi ya ukoloni.
10. Katika mfumo wa elimu tuweke msisitizo kuwa- jengea uwezo na umahiri wafundishaji jinsi ya kufundisha vizuri zaidi na kuwajengea uwezo wanafunzi namna ya kujifunza kwa ufahamu mpana na sio kufaulu tu mitihani.